Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA**

**IDD KITURE DHIDI YA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 010/2019**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, 5 Juni 2026:** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa Hukumu katika kesi ya *Idd Kiture dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Idd Kiture (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi). Wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Ukonga, Dar es Salaam, Tanzania, baada ya kusikilizwa kesi, kukutwa na hatia na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 kwa kosa la ubakaji wa mtoto mdogo na kwa kutenda kosa lisilo la kawaida. Alidai haki zake zilikiukwa wakati wa kuendeshwa kesi mbele ya mahakama za kitaifa.

Mjibu Maombi alitoa pingamizi dhidi ya mamlaka ya Mahakama kwa misingi miwili, Kwanza, kwamba Mahakama haijapewa mamlaka ya kuskiliza Maombi haya na pili, kwamba tafsiri na matumizi ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba) na Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki) haitoi mamlaka kwa Mahakama kumwachia huru Mleta Maombi.

Kuhusiana na pingamizi la kwanza, Mahakama ilirejelea kwamba chini ya Kifungu cha 3(1) cha Itifaki, ina mamlaka ya kuamua madai kuhusu tafsiri na matumizi ya Mkataba na hati nyingine za haki za binadamu zilizoidhinishwa na Mjibu Maombi.

Mahakama ilirejelea kwamba katika suala hilo, Mleta Maombi alidai kukiukwa kwa Vifungu vya 2, 3, 7(a), 7(c) na 7(d) vya Mkataba, hati ambayo Mjibu Maombi ameridhia. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi kuhusu mamlaka yake ya kisheria katika suala hili.

Kuhusiana na pingamizi la pili, kwamba Mahakama haikuwa na mamlaka ya kuamuru Mleta Maombi aachiliwe huru kutoka gerezani, ilirejelea kwamba Kifungu cha 27(1) cha Itifaki kinachomwezesha kutoa amri zinazofaa ili kuleta suluhu ya ukiukaji, ikiwa ni pamoja na kuachiliwa huru kwa mleta maombi kotoka gerezani, ili mradi ukiukaji unaodaiwa kufanywa umethibitishwa. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi kuhusu kipengele hiki na ikasisitiza kuwa ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi haya.

Ingawa vipengele vingine vya mamlaka yake havikupingwa na Mjibu Maombi, hata hivyo, Mahakama iliviangalia kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Mahakama (Kanuni za Mahakama). Kwa hivyo, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki ambacho kinaruhusu watu binafsi kuwasilisha Maombi dhidi yake kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Shauri kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Shauri hili kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa tarehe baada ya Shauri hili kuwasilishwa, mnamo tarehe 22 Machi 2019.

Mahakama pia ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki na ukiukaji ulitokana na kesi na hukumu ya Mleta Maombi, ambao ulifanyika baada

ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki. Aidha, Mleta Maombi anabaki gerezani kulingana na kile anachokiona kuwa mchakato usio wa haki, ukiukaji huo unachukuliwa kuwa unaendelea kikawaida. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo kwa sababu ukiukaji unaodaiwa kufanywa ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi. Kwa kuzingatia yote yaliyotajwa hapo juu, Mahakama iliona kwamba ina mamlaka ya kuamua Maombi haya.

Mahakama iliona kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zote zilizowasilishwa mbele yake. Katika Maombi haya, ilibainisha kwamba Mjibu Maombi alitoa pingamizi kwamba Mleta Maombi hakukamilisha taratibu za ndani zilizopo ndani ya mfumo wake wa kisheria kama ilivyoelezwa chini ya Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama. Hasa, kwamba endapo Mleta Maombi alihuzunishwa na hukumu ya Mahakama ya Rufaa, alipaswa kuwasilisha ombi la kupitia upya uamuzi wa Mahakama ya Rufaa kama ilivyoelezwa kwa mujibu wa Kanuni za Mahakama ya Rufaa. Kwa upande wake, Mleta Maombi alidai kwamba aliwasilisha ombi lake baada ya kukamilisha taratibu za ndani kwa kuwa kesi hiyo ilisikilizwa na kutupiliwa mbali na mahakama ya juu katika nchi ya Mjibu Maombi.

Mahakama, kwa kujibu pingamizi hili, iliona kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 56(5) cha Mkataba, ambacho masharti yake yametajwa tena katika Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za mahakama, maombi yoyote yaliyowasilishwa mbele yake lazima yatimize matakwa ya kutumia njia zote za utatuzi za ndani isipokuwa pale ambapo njia hizo hazipatikani, hazina ufanisi au kesi za ndani zinaendeshwa kwa muda mrefu isivyo lazima. Aidha, Mahakama ilibainisha kuwa kesi ya Mleta Maombi ilisikilizwa kikamilifu na Mahakama ya Wilaya ya Morogoro, Mahakama Kuu ya Dar es Salaam, na hatimaye Mahakama ya Rufaa ambazo zilitoa maamuzi yao tarehe 20 Julai 2010, tarehe 7 Septemba 2010; na tarehe 14 Novemba 2014, mtawalia. Kwa kuwa Mahakama ya Rufaa ni chombo cha juu zaidi cha mahakama ndani ya mfumo wa kisheria wa Mjibu Maombi, Mahakama ilibaini kuwa Mleta Maombi alikuwa amekamilisha taratibu za ndani.

Ikirejelea busara yake ya kisheria, Mahakama ilisisitiza kusema kwamba suluhu ya kupitia upya uamuzi wa Mahakama ya Rufaa kama ilivyoelezwa ndani ya sheria za Mjibu Maombi ilikuwa njia isiyo ya kawaida ambayo Mleta Maombi hakuhitaji kukamilisha kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 56(5) cha Mkataba na kama ilivyorudiwa katika Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama. Matokeo yake, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi la Mjibu Maombi kuhusu ukubalifu wa Maombi kulingana na kutokamilisha taratibu za ndani. Wakati ikiona kwamba hakuna pingamizi lililotolewa kuhusiana na matakwa mengine ya ukubalifu, hata hivyo, Mahakama ilitathmini vigezo vyote vya ukubalifu vilivyoainishwa katika Kanuni ya 50(2) ya Kanuni za Mahakama.

Mahakama ilibaini kwmaba Mleta Maombi alikuwa ametambuliwa kwa kwa jina katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta Maombi yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi haya yalitimiza Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama. Aidha, Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Shauri husika haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Shauri au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama. Maombi haya pia hayakutokana tu na habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama. Matokeo yake, Mahakama ilitangaza kuwa Maombi hayo yanakubalika.

Kwa kuangalia uzingatiaji wa sheria wa kesi hiyo, Mahakama iliangalia endapo Mjibu Maombi alikuwa amekiuka Vifungu vya 2, 3, 7 (1) (a), 7(1) (d) na 5 vya Mkataba, mtawalia kama inavyodaiwa na Mleta Maombi.

Kwa madai ya kwanza kwamba Waleta Maombi wana haki ya kutobaguliwa, kuwa na usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria kama ilivyoelezwa chini ya Vifungu vya 2 na 3 vya Mkataba, Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria kwamba mzigo wa uthibitisho wa ukiukaji wa haki za binadamu uko kwa mtu anayetoa madai, isipokuwa Mahakama iamue vinginevyo. Katika Maombi haya,

Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi alitoa madai hayo bila kuthibitisha madai yake. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali madai haya kwa kutokuwa na ushahidi kuhusiana na madai ya ukiukaji wa Kifungu cha 2 na 3 cha Mkataba.

Kwa kuzingatia madai ya pili ya Mleta Maombi kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki yake ya kukata rufaa kwenye vyombo vya kitaifa vyenye uwezo kama ilivyohakikishwa chini ya Kifungu cha 7(1)(a) cha Mkataba, Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria kwamba maelezo ya jumla kwamba haki imekiukwa hayatoshi, na uthibitisho zaidi unahitajika. Mahakama baada ya kubaini kwamba Mleta Maombi alishindwa kuonyesha jinsi haki hii ilivyovunjwa na pia ikibaini kwamba Mleta Maombi alikuwa ametumia haki yake ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa mahakama ya mwanzo hadi Mahakama ya Rufaa, ambayo ni Mahakama ya juu zaidi katika nchi ya Mjibu Maombi, ilibaini kwamba Mjibu Maombi hakukikuka haki ya Mleta Maombi ya kukata rufaa kwenda kwenye vyombo husika vya kitaifa iliyohakikishwa chini ya Kifungu cha 7(1)(a) cha Mkataba.

Kisha Mahakama iliangalia madai ya tatu ya Mleta Maombi kwamba alinyimwa uwakilishi wa kisheria wakati wa kuhojiwa kwake katika kituo cha polisi na wakati wote wa kusikilizwa kesi yake kinyume cha Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba. Mahakama iliona kwamba Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba hakionyeshi wazi haki ya kupata msaada wa kisheria bila malipo lakini kwamba Kifungu cha 14(3)(d) cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) ambacho Mjibu Maombi ni Nchi Mwanachama, kinaonyesha hivyo waziwazi.

Kutokana na kumbukumbu za uendeshaji wa kesi, na kutokana na maamuzi ya mahakama za ndani, Mahakama iliona kwamba Mleta Maombi hakupewa uwakilishi wa kisheria, ingawa alishtakiwa kwa kosa kubwa la ubakaji wa mtoto mdogo (mwenye umri wa miaka 12), ambalo lina adhabu ya kifungo cha miaka 30 baada ya kukutwa na hatia. Ikirejelea busara yake ya kisheria, Mahakama ilibaini kwamba katika hali kama hizo na kwa maslahi ya haki, msaada wa kisheria bila

malipo ulipaswa kutolewa na Mjibu Maombi endapo Mleta Maombi aliomba msaada huo, na hii haikupaswa kutegemea upatikanaji wa rasilimali fedha. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekiuka haki ya Mleta Maombi ya uwakilishi wa kisheria kama ilivyohakikishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba kama kinavyosomwa kwa pamoja na Kifungu cha 14(3)(d) cha ICCPR.

Kwa madai ya nne kwamba Mjibu Maombi alirefusha muda wa kesi ya Mleta Maombi, kinyume cha masharti ya Kifungu cha 7(1)(d) cha Mkataba, Mahakama iliona ni muhimu kutumia Kifungu cha 9(3) cha ICCPR, ingawa hakikutajwa na Mleta Maombi, kwa kuwa kilikuwa na maelezo ya wazi zaidi kuhusu haki hii. Katika kuzingatia madai haya, Mahakama iliainisha ucheleweshaji unaodaiwa kufanywa katika sehemu mbili, ambazo ni: muda wa kuwekwa kizuizini kabla ya kesi na ucheleweshaji katika kipindi chote cha kusikiliza kesi mbele ya mahakama za kitaifa.

Kuhusu kuwekwa kizuizini kabla ya kusikiliza kesi, Mahakama ilibaini kwamba hali hii haikuzidi saa 48, muda ambao unachukuliwa kuwa unafaa kutokana na uzito wa kosa la ubakaji na matokeo ya upelelezi na uchunguzi wa kitabibu ambao ulipaswa kufanywa na mamlaka ya polisi. Kwa kuzingatia yaliyotajwa hapo juu, Mahakama ilibaini kwamba Mjibu Maombi hakuvunja haki ya Mleta Maombi ya kushtakiwa ndani ya muda unaofaa kama ilivyohakikishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(d) cha Mkataba kama kinavyosomwa pamoja na Kifungu cha 9(3) cha ICCPR kuhusiana na kuwekwa kizuizini kabla ya kufikishwa mahakamani.

Kuhusu madai ya kucheleweshwa kwa kesi zote mbele ya mahakama za ndani kuanzia Mahakama ya Wilaya ya Morogoro hadi kumalizika kwa kesi hiyo, Mahakama ya Rufaa ilipotoa uamuzi wake, kipindi cha miaka sita (6), miezi mitano (5) na siku moja (1) kilikuwa kimepita. Vivyo hivyo, Mahakama ilirejelea busara yake ya kisheria kwamba ingawa ucheleweshaji fulani unaweza kuhusishwa na

maombi ya kiutaratibu yanayofanywa na Mleta Maombi, jukumu la kuhakikisha kwamba haki inatolewa bila kuchelewa sana mwishowe liko kwa Serikali.

Mahakama iliona kwamba kesi hiyo haikuwa ngumu kwani haikuhitaji kutafuta ushahidi au kuangalia ushahidi maalumu kama vile kuchukua sampuli za DNA, wakati huo ripoti ya kitabibu ya mwathiriwa aliyebakwa iliwasilishwa kama ushahidi na upande wa mashtaka, ambao haukupingwa na Mleta Maombi. Aidha, upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi 4 wakati Mleta Maombi alikuwa na shahidi 1 tu ambaye alitoa ushahidi. Mahakama pia iliona kwamba kesi hiyo iliahirishwa mara kadhaa wakati wa kuisikiliza mbele ya Mahakama ya Wilaya, kwa ombi la Mjibu Maombi. Aidha, Mahakama ya Wilaya iliruhusu maombi ya Mleta Maombi *kuanza upya* kesi hiyo wakati jaji mpya atakaposimamia kesi hiyo. Hii ilisababisha mashahidi wote wa mashtaka kutoa ushahidi upya ambao hapo awali walitoa ushahidi.

Kwa hivyo, Mahakama ilibaini kwamba Mjibu Maombi hakuvunja haki ya Mleta Maombi ya kushtakiwa ndani ya muda unaofaa uliohakikishwa chini ya Kifungu cha 7(1)(d) cha Mkataba kuhusu kipindi cha kusikiliza kesi mbele ya mahakama za ndani cha miaka sita, miezi mitano na siku moja.

Kuhusu ukiukaji wa tano wa madai ya Mleta Maombi kuhusu haki yake ya kusikilizwa kwa haki kinyume cha Kifungu cha 7(1) cha Mkataba kwa sababu alihukumiwa kwa msingi wa hati ya mashtaka isiyo na maelezo sahihi, Mjibu Maombi aliwasilisha kwamba, madai hayo yalihusu masuala ya uthibitisho ambayo Mahakama hii haina mamlaka ya kuyaangalia. Mjibu Maombi alidai kwamba endapo Mahakama itaangalia masuala ya uthibitisho, itakuwa imeketi kama mahakama ya rufaa kuhusiana na masuala ambayo tayari yaliamuliwa na mahakama ya juu katika nchi ya Mjibu Maombi, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania. Mahakama iliona kwamba Kifungu cha 7(1) cha Mkataba kinahakikisha ulinzi wa haki za kusikilizwa kwa haki, hata hivyo, iliona ni muhimu kutumia Kifungu cha 14 cha ICCPR, ambacho kinashughulikia haki hiyo kwa undani zaidi. Mahakama ilibaini kwamba Mjibu Maombi kushindwa kurekodi kosa kwenye hati ya mashtaka

ya Mleta Maombi lilikuwa kosa la kiutaratibu, ambalo hata hivyo, halikusababisha kupotoshwa kwa haki, kwa kuwa Mleta Maombi aliweza kuelewa kosa ambalo alishtakiwa pia kukata rufaa. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi hakukiuka haki ya Mleta Maombi ya kusikilizwa kwa haki iliyohakikishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) cha Mkataba kama kinavyosomwa pamoja na Kifungu cha 14 cha ICCPR kuhusiana na madai ya kumshtaki Mleta Maombi kwa kutumia hati ya mashtaka isiyo na maelezo sahihi.

Kuhusu ukiukaji wa sita na wa mwisho unaodaiwa kufanywa kuhusu haki ya utu ya Mleta Maombi, inayolindwa kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Mkataba, Mleta Maombi alidai kwamba alinyanyaswa na kupigwa alipokuwa akihojiwa na polisi alipokuwa akirekodi maelezo yake. Mahakama ilisisitiza busara yake ya kisheria, kwamba mzigo wa kuthibitisha madai ya ukiukaji wa haki ya binadamu uko kwa mtu anayetoa madai hayo. Ingawa havikutajwa na Mleta Maombi, Mahakama ilibaini kutumia Vifungu vya 1 na 12 vya Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Mateso na Matendo Mengine ya Ukatili, Unyama au Udhalilishaji au Adhabu (UNCAT), ambavyo vinaelezea haki hiyo kwa undani zaidi. Mahakama ilirejelea kwamba maelezo ya jumla kwamba haki imekiukwa hayatoshi kuthibistisha kuwa kuna ukiukaji. Kwa kuwa Mleta Maombi alikuwa hajatoa uthibitisho wa ukiukaji wa haki yake ya utu, Mahakama iliona kwamba Mjibu Maombi hakukiuka haki ya Mleta Maombi ya kutotendewa ukatili, unyama na udhalilishaji kama ilivyoelezwa chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba na Vifungu vya 1 na 12 vya UNCAT.

Kuhusu fidia, Mahakama ilisisitiza kwamba ikiwa ukiukaji umebainishwa, Kifungu cha 27(1) cha Itifaki kinaipa uwezo wa kuamuru suluhu inayofaa. Katika hali hiyo ukiukaji wa haki ya Mleta Maombi ya kupata uwakilishi wa kisheria bila malipo kama ilivyohakikishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(c) cha Mkataba kikisomwa pamoja na Kifungu cha 14(3) (d) cha ICCPR ulibainishwa. Hata hivyo, Mleta Maombi alishindwa kuweka uhusiano kati ya ukiukaji uliobainishwa na hasara iliyosababishwa. Kwa hivyo, Mahakama ilikataa madai haya ya fidia ya hasara ya mali. Hata hivyo, Mahakama ilimpa Mleta Maombi kiasi cha Shilingi za Tanzania

mia tano (Sh. 500) kama ishara ya kutambua hasara ya kimaadili inayotokana na ukiukaji wa haki ya kuwakilishwa na wakili bila malipo.

Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mleta Maombi kuhusu kuondoa hatia na hukumu yake na kumuweka huru, ikisema kwamba ingawa ukiukaji wa haki ya Mleta Maombi ya kupata msaada wa kisheria bila malipo ulibainishwa, haukuwa na athari kwenye hatia, hukumu na kifungo cha Mleta Maombi. Kwa hivyo, hakukuwa na sababu ya kuhalalisha au kulazimisha kufuta hatia na kubatilisha hukumu na kumweka huru Mleta Maombi.

Kuhusu utekelezaji na utoaji taarifa, Mahakama, iliamuru Mjibu Maombi awasilishe ripoti kwake, ndani ya miezi sita (6) tangu tarehe ya taarifa ya hukumu kutolewa, kuhusu hali ya utekelezaji wa maagizo kila baada ya miezi sita (6), hadi Mahakama itakapoona kuwa kumekuwa na utekelezaji kamili.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

**<u>Maelezo zaidi</u>**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0102019

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe kupitia registrar@african-court.org

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote

cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Maelezo ya ziada yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya Mahakama kupitia www.african-court.org.